JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO

(MAENDELEO YA JAMII)



# MWONGOZO WA UHAMASISHAJI UJENZI WA NYUMBA BORA NGAZI YA JAMII

DISEMBA, 2019

## YALIYOMO


Yaliyomo ........ i
Vifupisho ........ iii
FASIRI YA MANENO ........ iv
DIBAJI ........ v
UTANGULIZI ........ 1
I. Usuli ........ 1
II. Lengo la Mwongozo ........ 2
III. Malengo Mahsusi ........ 2
IV. Walengwa wa Mwongozo ........ 3
V. Muundo wa Mwongozo ........ 3
SURA YA KWANZA: MAELEKEZO YA KUANDAA NA KUTEKELEZA KAMPENI ........ 4
1.1 Hatua ya Kwanza: Kuandaa Kampeni ........ 4
1.1.2 Uchambuzi wa Hali ya Kiuchumi na Kijamii ........ 4
1.1.3 Uainishaji wa Wadau ........ 4
1.1.4 Uainishaji wa Raslimali ........ 5
1.1.3 Mbinu zitakazotumika ........ 5
1.2 Hatua ya Pili: Utambulisho na Uhamasishaji wa Kampeni ........ 5
1.3 Hatua ya Tatu: Uhamasishaji wa Kampeni kwa Makundi mbalimbali ........ 6
1.3.1 Makundi mbalimbali ........ 6
1.3.2 Makampuni au Taasisi za Uwekezaji Ngazi ya Jamii ........ 7
1.3.4 Asasi za Kiraia ........ 8
1.4 Kutoa ushauri wa Kitaalam ........ 8
1.5 Masuala ya Kuzingatia wakati wa kufanya Kampeni ........ 8
SURA YA PILI: MGAWANYO WA MAJUKUMU ........ 9
2.1 Utangulizi ........ 9
2.2 Mgawanyo wa Majukumu kwa Ngazi Mbali mbali ........ 10
2.2.1 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii) ........ 9
2.2.2 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI) ........ 9
2.2.3 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ........ 9
2.2.4 Taasisi za Mafunzi ........ 10
2.2.5 Mkoa ........ 10
2.2.6 Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) ........ 10
2.2.7 Kata ........ 11
2.2.8 Asasi za Kiraia ........ 11
2.2.9 Sekta Binafsi ........ 11

Sura Ya Tatu: Ufuatiliaji, Tathimini Na Utoaji Wa Taarifa....13
3.1 Ufuatiliaji....19
3.2 Tathmini....193
3.2.1 Masuala Yatakayotathiminiwa....13
3.3 Uenezi wa Kampeni....19
4.0 Hitimisho.... 14
5.0 Viambatisho....15

5.1 Kiambatisho Na. 1: Dodoso la Kukusanyia Takwimu za Kiuchumi na Kijami...15
5.2 Kiambatisho Na. 2: Zana za Kukusanyia Taarifa zaMakazi.... 17

## VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| CBO's | - | Community Based Organisations (Vikundi vya Kijamii) |
| CSO's | - | Civil Society Organisation (Mashirika ya Kiraia) |
| OR - TAMISEMI | - | Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| VICOBA | - | Community Banks (Benki za Kijamii za Vijijini) |
| SACCOs | - | Savings and Cooperetive Credit Organisation (Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo) |

## FASIRI YA MANENO

### Nyumba Bora

Ni ile iliyojengwa kwa mpangilio mzuri na kutumia vifaa vya ujenzi vyenye ubora, yenye madirisha yanayopitisha mwanga na hewa ya kutosha, iliyoezekwa vizuri na yenye choo bora.

### Nyumba Bora ya Gharama Nafuu

Kwa mujibu wa makadirio ya wasanifu majengo, nyumba bora ya gharama nafuu na teknolojia rahisi inagharimu kati ya shilingi 9,500,000 hadi 12,579,330/= kwa nyumba ya vyumba tatu, sebule, jiko na choo kutegemeana na upatikanaji wa vifaa vya ujenzi katika eneo husika

### Kampeni ya Nyumba Bora

Kampeni ya kuamsha ari ya jamii kuboresha au kujenga nyumba bora zenye gharama nafuu zinazotumia teknolojia rahisi na sahihi itakayoratibiwa na wataalam wa maendeleo ya jamii nchini.

### Teknolojia Rahisi

Teknolojia rahisi ni zile zinazotokana na raslimali zinazopatikana ndani na nje ya jamii katika ujenzi na uboreshaji wa makazi kama vile matofali yanayotumia saruji na udongo kidogo, matofali ya kuchoma, vigae vya kutengenezwa kwa udongo na kamba ya mkonge au udongo wa jasi (Drywall) kwa wale wenye kipato cha wastani na nyinginezo.

### Mifumo Asili ya Kufanya Kazi Pamoja Kwenye Jamii

Ni utaratibu wa asili wa kusaidiana kufanya kazi za kimaendeleo miongoni mwa wanajamii. Utaratibu huu upo katika makabila mbalimbali na ujulikana kwa majina tofauti mfano "Mgohe" kwa Wahehe, "Msaragambo" kwa Wapare, "Embesi" kwa Wameru, "Okweiyayo" kwa Wahaya, "Kirundio" kwa Wachaga, "Isalenge" kwa Wasukuma, "Lisaga" kwa Wazanaki, "Saragata" kwa Wagogo, "oluguyo" kwa Wajita, "Ngokela" kwa Wanyasa na Ireka kwa Wanyaturu.

## DIBAJI

Nyumba bora ni hitaji la msingi la mwanadamu. Kampeni ya Kitaifa imezingatia umuhimu huo na imejikita katika kuhamasisha wananchi kuhusu ujenzi nyumba bora kwa kutumia teknolojia rahisi na gharama nafuu. Kampeni hii inakusudia kufanya mageuzi ya kifikra na mtizamo wa jamii ya watanzania kuendelea na utamaduni wa kupenda kushiriki katika shughuli za kujiletea maendeleo yenye matokeo yanayoonekana kama inavyosisitizwa na Serikali ya Awamu ya Tano. Kampeni hii ni ya kipekee kwa kuwa inakusudia kutumia mifumo ya asili ya kufanya kazi pamoja na kugusa mahitaji ya mtu binafsi katika kuboresha makazi kwa kutumia teknolojia rahisi na ya gharama nafuu ili kukuza ushiriki, umiliki na dhana ya kuacha utegemezi.

Kampeni hii ni utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996) ibara ya 17 (d – (iv)) na Ilani ya uchaguzi ya mwaka 2015 - 2020 Ibara ya 4 (c). Kutokana na Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/2018 unaonesha kuwa asilimia 15.9 ya kaya nchini bado zinaishi kwenye nyumba duni (nyasi na udongo) zilizojengwa na kuezekwa kwa vifaa visivyo bora. Sababu zinazochangia makazi duni ni pamoja na kutoelewa umuhimu wa makazi bora, kutomudu gharama kubwa za vifaa vya ujenzi na uelewa mdogo kuhusu teknolojia rahisi za ujenzi zenye gharama nafuu. Matokeo ya utafiti huo yameibua umuhimu wa kufanya Kampeni ya kuamsha ari ya jamii nchi nzima kuboresha makazi yao kwa kutumia teknolojia rahisi na gharama nafuu.

Mwongozo huu umeandaliwa ili kujenga uelewa wa pamoja wa namna ya kutekeleza kampeni. Aidha, Mwongozo unaelezea majukumu ya wataalam wa maendeleo ya jamii na wadau katika kutekeleza Kampeni ikiwemo maelekezo ya Kisera, Mipango na Programu za Kitaifa kuhusu uboreshaji makazi, mifumo ya asili ya kufanya kazi pamoja na hatua zinazopaswa kufuatwa katika kutekeleza Kampeni. Hivyo, Matokeo ya utekelezaji wa mwongozo huu ni kubadilika kifikra na mtizamo kuhusu ujenzi wa nyumba bora ili jamii iishi kwenye makazi bora.

Natoa wito kwa wadau wote kuutumia mwongozo huu ili kuwezesha kufikia lengo la kampeni hii ambayo itawezesha jamii kuishi katika makazi bora.

**Dkt J.K. Jingu**
**KATIBU MKUU**
**UTANGULIZI**

## UTANGULIZI

### I. Usuli

Nyumba bora ni ile iliyojengwa kwa mpangilio mzuri na kutumia vifaa vya ujenzi vyenye ubora, yenye madirisha yanayopitisha mwanga na hewa ya kutosha, iliyoezekwa vizuri na yenye choo bora.

Tanzania bado ina asilimia 15.9 ya kaya zinazoishi katika nyumba duni ukilinganishwa na asilimia 84.1 zinazoishi katika nyumba zilizojengwa kwa vifaa vya kisasa kama vile zege, mawe, saruji na vyuma. Aidha, Kwa mujibu wa Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/2018, nyumba duni ni nyingi zaidi maeneo ya vijijini ukilinganisha na mijini. Kwa upande wa vijijini nyumba zenye paa duni ni asilimia ya 23.4, asilimia 29.5 Kuta hazijasilibiwa na asilimia 67.9 hazijasakafiwa (Ofisi ya Taifa ya TAKWIMU,2017/2018). Mikoa kumi inayoongoza kwa makazi duni ni Lindi, Kagera, Tanga, Tabora na Pwani, Arusha, Kigoma, Singida, Mtwara na Katavi. Miongoni mwa sababu zinazochangia makazi duni ni pamoja na kutoelewa umuhimu wa makazi bora, kipato kidogo kumudu gharama za vifaa vya ujenzi na uelewa mdogo kuhusu teknolojia rahisi za ujenzi na zenye gharama nafuu.

Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012, inaonesha kuwa Idadi ya watu Tanzania ilikuwa watu milioni 44.9. Kwa kuzingatia ukuaji wa Idadi ya watu ambao ni asilimia 2.7. Kufikia mwaka 2018 Tanzania inakadiriwa kuwa na watu wapatao millioni 54.2 ambapo wanaume ni milioni 26.5 sawa (asilimia 49) na wanawake milioni 27.6 sawa na (asilimia 51). Kwa upande mwingine, ukuaji wa pato la Taifa umeongezeka na kufikia asilimia 7.0 (Ofisi ya Taifa ya Takwimu 2018). Pamoja na mafanikio ya ukuaji wa uchumi jamii bado inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwemo makazi duni. Matokeo ya utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya Binafsi wa Mwaka 2017/2018 na ongezo la idadi ya watu kwa pamoja vimechangia umuhimu wa kufanya Kampeni ya kuamsha ari ya jamii nchi nzima kuboresha makazi yao kwa kutumia teknolojia rahisi na gharama nafuu kama ilivyoainishwa kwenye Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996) kifungu cha 17 (v).

Kampeni hii ni ya kipekee kwa kuwa itatumia mifumo ya asili ya kusaidiana ili kushughulikia mahitaji ya mtu binafsi katika kuboresha makazi kwa lengo la kukuza ushiriki, umiliki na dhana ya kuacha utegemezi. Kaulimbiu ya Kampeni hii

ni "**Piga Kazi Boresha Makazi**". Kampeni inazingatia uzoefu wa Kampeni za Kimataifa na Kitaifa ambazo zimefanyika tangu kupatikana kwa uhuru wa Tanzania Mwaka 1961. Mfano wa Kampeni za Kimataifa ni pamoja na Kampeni ya kitaifa ya Rwanda iliyopewa jina la "**bye bye Nyakatsi**" ikimaanisha "**Kwa Heri Nyumba za Nyasi**" ya Mwaka 2009. Kitaifa ni pamoja na Kampeni za "Uhuru na Kazi", "Uhuru na Maendeleo", "Uhuru na Umoja" na "Kilimo cha Kufa na Kupona" ambapo ziliwezesha mwananchi kushiriki kikamilifu kutatua changamoto zinazokabili jamii na mtu mmoja mmoja kupitia Mipango shirikishi, Miradi na Programu.

Kampeni hii inalenga kufanya mageuzi ya kifikra na mtizamo wa jamii kuhusu makazi bora. Malengo Mahsusi ni pamoja na; (i) Kuamsha ari ya jamii katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara kusaidiana na kushirikiana katika shughuli za ujenzi wa nyumba bora. (ii) Kuhamasisha wananchi kutumia rasilimali na teknolojia rahisi na sahihi katika ujenzi wa nyumba bora. (iii) Kuelimisha jamii kutumia kikamilifu fursa zilizopo kupitia vikundi vya kusaidiana, VICOBA, SACCOS na Benki za Kijamii, Vyama vya Ushirika wa Nyumba na Asasi za Kiraia katika kuboresha makazi yao na (iv) Kuhamasisha jamii, makampuni kujitolea katika kuboresha makazi ya kaya duni zenye uhitaji maalum wa nyumba bora. Aidha, Matokeo tarajiwa ni: (i) Kuongezeka kwa kaya zinazoishi katika nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi na (ii) Kuongezeka kwa mwamko wa kusaidiana miongoni katika ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu zinazotumia teknolojia rahisi.

Kwa kuwa Kampeni itatekelezwa Tanzania Bara, ni vema ukaandaliwa mwongozo utakaowezesha wataalam wa Maendeleo ya Jamii na wadau wengine kutekeleza Kampeni kwa kuzingatia mambo ya msingi yanayoanishwa kwenye mwongozo.

### II. Lengo la Mwongozo

Mwongozo huu kupitia Kampeni unakusudia kujenga uwezo na kubadili fikra na mtizamo wa makundi mbali mbali kwenye jamii kuboresha makazi.

### III. Malengo Mahsusi ni;

(i) Kujenga uelewa wa pamoja wa kuleta mabadiliko ya kifikra na mtizamo wa jamii kuhusu makazi bora.

(ii) Kuwa na mfumo unaofanana wa kutekeleza Kampeni ya kuboresha makazi miongoni mwa wadau

(iii) Kuwezesha Viongozi, Wataalam wa Maendeleo ya Jamii,

a. ASASI za Kiraia, Wafanya biashara na Makampuni kutekeleza Kampeni ya kuboresha makazi hatua kwa hatua

## IV. Walengwa wa Mwongozo

Mwongozo huu umelenga kutumiwa na Wataalam wa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata, Halmashauri, Mkoa, Asasi za Kiraia, Wadau wa Maendeleo na Viongozi watakaoshiriki kwenye Kampeni ya kuboresha makazi.

## V. Muundo wa Mwongozo

Mwongozo huu umegawanyika katika Sura kuu Tatu. Sura ya kwanza inahusu maelekezo ya kuandaa na kutekeleza kampeni na imejumuisha hatua za kufuatwa kabla na wakati wa utekelezaji wa Kampeni. Sura ya Pili, inaelezea mgawanyo wa majukumu ya utekelezaji kwa wadau mbalimbali ili kurahisisha utekelezaji wa Kampeni. Sura ya Tatu inahusu Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa. Katika hatua hii Mwongozo umeanisha njia zitakazotumika katika ufuatiliaji, Viashiria na masuala yatakayotathminiwa kuhusu Kampeni. Pia inaelekeza utaratibu wa utoaji wa taarifa.

## SURA YA KWANZA

## 1.0 MAELEKEZO YA KUANDAA NA KUTEKELEZA KAMPENI

Sura ya hii inaainisha jinsi Kampeni itakavyotekelezwa hatua kwa hatua kama zilivyoanishwa kwenye Mwongozo huu. Izingatiwe kuwa jamii zimetofautiana kiuchumi, kiutamaduni na mazingira, hivyo basi ni muhimu watumiaji wakaifahamu vyema jamii wanayoiendea na kutumia mifumo iliyopo ili kufanikisha Kampeni. Hatua za kufuata ni kama ifuatavyo:

### 1.1 Hatua ya Kwanza: Kuandaa Kampeni

#### 1.1.1 Kuandaa ratiba ya utekelezaji wa Kampeni

Ratiba ya kazi ni nyenzo muhimu katika kufikia ufanisi. Kabla ya kuanza utekelezaji wa Kampeni itapaswa kuandaa ratiba itakayoongoza utekelezaji wa kampeni hatua kwa hatua. Ratiba hiyo iainishe shughuli zinazokusudiwa kufanyika, atakayehusika, muda wa kufanyika na raslimali zinazohitajika.

#### 1.1.2 Uchambuzi wa Hali ya Kiuchumi na Kijamii

Katika kuandaa Kampeni, Wataalam wanatakiwa kukusanya taarifa na takwimu za hali ya kiuchumi na kijamii zitakazosaidia katika kutambua Idadi ya nyumba za udongo, nyumba zilizoezekwa kwa nyasi au udongo (Tembe) na Idadi ya watu wenye mahitaji maalumu kuhusu makazi.

Pia inatakiwa kupata takwimu za hali ya kipato ili kujua wenye kipato cha juu lakini wanaoishi kwenye makazi duni, wenye kipato cha kati na wenye kipato cha chini. Vikundi vya kusaidiana vilivyopo na taratibu zao; vikundi vya VICOBA, SACCOs vilivyopo, vikosi vya ujenzi vilivyopo kwenye jamii, teknolojia za ujenzi wa nyumba zilizopo kwenye jamii, Kamati zilizopo, Mpango wa matumizi bora ya ardhi, upatikanaji wa vifaa vya ujenzi, shughuli za uchumi zilizopo kijijini na mifumo ya asili ya jamii ya kusaidiana.

#### 1.1.3 Uainishaji wa Wadau

Taarifa hizi ni muhimu na zitasaidia kupambanua mbinu nzuri ya kuifikia jamii na kufanikisha kampeni. Uchambuzi utasaidia kuelewa utayari wa jamii katika kazi za kusaidiana, makundi yenye ushawishi yatakavyotumika kufanikisha Kampeni, utayari wa viongozi kuwa mabalozi wa kufanikisha Kampeni. Vilevile uchambuzi wa Makundi Mbalimbali kwenye jamii utasaidia kujua watu wenye kipato cha

juu wanaoishi kwenye makazi duni, wenye kipato cha kati wanaoishi katika makazi duni na wana fursa za kuboresha makazi kupitia VICOBA, SACCOs, Benki za Kijamii na wenye kipato duni na hawana uwezo wa kujenga nyumba bora. Aidha, utasaidia kuibua mila nzuri zinazoweza kutumika kufanikisha Kampeni na pia mila kandamizi zilizopo zinazoweza kwakwamisha kampeni ili zishughulikiwe wakati wa Kampeni.

### 1.1.4 Uainishaji wa raslimali kwa ajili ya kutekeleza Kampeni

Kampeni hii itatekelezwa katika mazingira tofauti, yenye mila na desturi tofauti, hali ya kipato tofauti na mwitikio wa jamii kwenye maendeleo na kujitolea tofauti. Aidha, Kampeni hii ni tofauti na zile zenye mlengo wa kutatua changamoto za kijamii kwa ujumla wake bali inalenga kuboresha makazi ya mtu binafsi ambalo ni jukumu la mhusika mwenyewe.Hivyo, raslimali zinazohitajika kwa ajili ya kutekeleza kampeni zianishwe na kujulikana. Aidha, mbinu mbalimbali za kuwezesha kupatikana kwa raslimali zitumike katika kufanikisha kampeni.

### 1.1.5 Mbinu zitakazotumika

Mbinu zitakazotumika katika Kampeni zianishwe ikijumuisha:-

(i) Kupitia taarifa za tafiti, utekelezaji na machapisho kupata takwimu za awali zenye mahusiano na kampeni

(ii) Kukusanya taarifa moja kwa moja kutoka kwa walengwa kwa kutumia mbinu shirikishi kama: ramani ya rasilimali ili kutambua rasilimali na fursa za kuboresha makazi zilizopo kijijini: majadiliano ya kundi lengwa (focus group discussion) jadili na makundi mahsusi kama Vikundi vya uzalishaji vya wanawake na vijana, vikundi vya VICOBA, Wanachama wa SACCOs, Vikosi vya Ujenzi, Watu Mashuhuri Kijijini, Viongozi wa kiroho wa madhehebu ya Kiislam na Kikiristo;

(iii) Kufanya Kataa ya njia ili kutambua hali ya makazi, fursa zilizopo na vikwazo vya kushughulikia; washiriki wawe ni wazoefu wanaojua kijiji au mtaa vizuri; Miduara ya Mahusiano (Venn Diagram) zana hii itasaidia kujua mahusiano na makundi yenye ushawishi kwenye jamii ili yatumike na nyingine ambazo utaona zinafaa.

## 1.2 Hatua ya Pili: Utekelezaji wa Kampeni

### 1.2.1 Utambulisho na Uhamasishaji wa Kampeni

Kwa kutumia Mwongozo wataalam wa (Maendeleo ya Jamii, Afya, Mazingira,

Wahandisi wa ujenzi, Ardhi na Mipango Miji) kwa pamoja watafanya mikutano ya Mitaa au Vijiji kwa ajili ya kutambulisha Kampeni na dhana ya kusaidiana katika ujenzi wa nyumba bora. Kabla ya mikutano ya Vijiji/Mtaa utambulisho na uhamasishaji wa Kampeni ufanyike kwanza kwa viongozi wa Halmashauri ya Kijiji/ Kamati ya Mtaa ili kujenga uelewa wa pamoja kuhusu Kampeni. Lengo kuu la kukutanisha viongozi ni kutoa elimu kwao ili waelewe umuhimu wa nyumba bora

Viongozi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wandae mikutano ya hadhara ya vijiji/mtaa kwa ajili ya utambulisho na uhamasishaji wa Kampeni kwa jamii. Uhamasishaji ufanyike kwa kuzingatia mifumo ya asili ya kusaidiana iliyopo kwenye jamii mfano "Mgohe" kwa Wahehe, "Msaragambo" kwa Wapare, "Embesi" kwa Wameru, "Okweiyayo" kwa Wahaya, "Kirundio" kwa Wachaga, "Isalenge" kwa Wasukuma, "Lisaga" kwa Wazaramo, "Saragata" kwa Wagogo na Ireka kwa Wanyaturu.

Endapo katika Mkutano itadhihirika kuwa kuna mwanajamii/wanajamii wenye makazi duni na wanahitaji msaada wa nguvu za pamoja za kuwasaidia waweze kuwa na makazi bora, utaratibu wa namna ya kuwasaida uwekwe na jamii yenyewe kwa kupanga ratiba na kuitekeleza.

Baada ya Mikutano ya utambulisho mtaalam au timu ya uhamasishaji wakutane na makundi ya watu mashuhuri kwenye eneo husika, Mafundi, vijana, vikundi vya wanawake na waendesha bodaboda na viongozi wa dini ili kujadili namna makundi haya yatakavyoshiriki katika kutekeleza kampeni ya kuboresha makazi kwa kuzingatia taarifa zilizokusanywa katika hatua ya kwanza.

### 1.3 Hatua ya Tatu: Uhamasishaji wa Kampeni kwa Makundi mbalimbali

#### 1.3.1 Uhamasishaji kwa makundi mbalimbali

Kwa kutumia taarifa zilizopatikana hatua ya kwanza, fanya majadiliano na vikundi mbali mbali vikiwemo vikundi vya uzalishaji vya vijana, wanawake, Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCOs) na Benki za Kijamii Vijijini (VICOBA). Makundi haya ni ya kimkakati kwa kuwa yana fursa ya kupata rasilimali za kuboresha au kujenga nyumba bora kupitia utaratibu wao wa kuweka na kukopa na tayari yana mfumo wa kufanya kazi pamoja.

Mtaalam atumie fursa kuibua mjadala utakaowezesha makundi hayo kujadili, kupendekeza na kuchukua hatua ya kujenga au kuboresha makazi yao kwa kutumia fursa walizo nazo katika vikundi vyao, ikiwemo fedha kwa ajili ya kununulia vifaa vya ujenzi kama bati, saruji, milango, madirisha na vifaa vya ujenzi vinavyopatikana kwenye jamii ambavyo ni matofali, mchanga, mawe na mbao za kuezekea. Ni vyema wakatambua kuwa uzalishaji unaenda sambasamba na kuboresha maisha yao.



### 1.3.2 Makampuni au Taasisi za Uwekezaji Ngazi ya Jamii

Makampuni au Taasisi zilizopo ndani na nje ya Tanzania zinazofanya kazi za uzalishaji kwenye maeneo ya jamii yana utaratibu wa kusaidia kazi za maendeleo kwenye jamii zinazozunguka (Corporate Social Responsibility). Mtaalam atumie Mwongozo kushawishi Makampuni au Taasisi hizo kuchangia vifaa vya ujenzi kama saruji, bati, mbao, misumari na nondo kwa ajili kujenga nyumba za wenye uhitaji au kutoa motisha kwa walioanza ujenzi wa nyumba bora.

Kwa kuzingatia taarifa ulizopata kwenye hatua ya kwanza kundi la wenye kipato cha chini linaweza kuwa na wahitaji ambao hawana uwezo wa kujijengea nyumba wenyewe, hivyo basi unaweza kushawishi jamii kwa njia ya kujitolea kushiriki kuandaa vifaa vya ujenzi ngazi ya jamii kama mchanga, tofali, mawe na miti au mbao za kuezekea. Makampuni au taasisi ziombwe kuchangia vifaa kama bati, misumari, saruji, nondo, milango na madirisha. Pia makampuni yanaweza kuombwa kufanya ujenzi wa nyumba nzima ya mfano kwa kaya zenye uhitaji maalum.

Endapo itatokea vimepatikana vifaa vingi zaidi kama bati na saruji utaratibu unaweza kuwekwa wa kushindanisha wale watakaojitokeza kwa mara ya kwanza kujenga nyumba bora waweze kupewa hata bati tano za kuanzia au zaidi kulingana na rasilimali zilizopatikana kutoka kwa wadau.

### 1.3.4 Asasi za Kiraia

Kwa upande mwingine Asasi za Kiraia (CSOs) na vikundi vya kijamii (CBOs) zinazojishughulisha na uboreshaji wa makazi zishawishiwe ili zishiriki katika uhamasishaji na kuchangia utaalam wa kuamsha ari, kusaidia maandiko ya kupata rasimali au vifaa vya ujenzi au kujenga nyumba bora za mfano ili kuelimisha jamii. Izingatiwe kuwa Kampeni hii hailengi hamasa tu bali hamasa ijumuishe na matokeo ya nyumba bora zilizojengwa au kuboreshwa.

### 1.5 Kutoa ushauri wa Kitaalam

Katika kipindi cha utekelezaji wa Kampeni jamii itahitaji msaada wa ushauri wa kiufundi kuhusu ujenzi wa nyumba bora. Timu za wataalam ngazi ya Halmashauri wakiwemo wataalam wa Maendeleo ya Jamii, Wataalam wa Ardhi na Mipango Miji na Wahandisi wa ujenzi watahusika katika kutoa ushauri huo kwa kufanya ziara za kuwatembelea wananchi kwenye maeneo yao.

### 1.5 Masuala ya Kuzingatia wakati wa kufanya Kampeni

(i) Usimamizi wa raslimali iliyopatikana kwa ajili ya kufanya kampeni
(ii) Ushirikiano na Sekta za Umma na Binafsi

# SURA YA PILI

# MGAWANYO WA MAJUKUMU

## 2.1 Utangulizi

Wadau mbali mbali watahusika katika kutekeleza Kampeni hususani kutoa elimu na kueneza matumizi ya teknolojia mbali mbali, kuwezesha upatikanaji wa rasimali au vifaa vya ujenzi ngazi ya jamii na nje ya jamii na kusambaza huduma ya nishati ya umeme na maji.

## 2.2 Mgawanyo wa Majukumu kwa Ngazi Mbali mbali

Mwongozo utatekelezwa na wadau mbalimbali katika ngazi ya Taifa hadi Kijiji/mtaa.

### 2.2.1 Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii)

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kutoa miongozo ya Kisera katika uratibu na utekeleza wa Kampeni,
(ii) Kujenga uwezo wa wataalam na wadau katika kutekeleza Kampeni,
(iii) Kutafuta raslimali za kusaidia utekelezaji wa Kampeni
(iv) Kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa Kampeni, na
(v) Kuhakikisha utekelezaji wa Kampeni unafanyika kwa kuzingatia Sera, Miongozo na Sheria za Nchi kuhusu ujenzi wa Makazi.

### 2.2.2 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR TAMISEMI)

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia utekelezaji wa Kampeni katika ngazi ya Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa,
(ii) Kuhakikisha Halmashauri zinatenga bajeti ya utekelezaji wa kampeni,
(iii) Kujumuisha taarifa za utekelezaji wa kampeni kutoka ngazi ya Mkoa, na
(iv) Kufuatilia utekelezaji wa Kampeni (hii itangulie)

### 2.2.3 Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Wizara hii itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kutoa utaalamu wa kiufundi kuhusu uboreshaji wa makazi na kushiriki katika ufuatiliaji na tathmini ya Kampeni, na

(ii) Kushirikiana na mamlaka husika kupanga matumizi bora ya ardhi ili kuzuia ujenzi holela

2.2.4 **Taasisi za Mafunzo**

Taasisi za Mafunzo zitakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kupitia mifumo yake ya kufanya kazi na jamii (Community Engagement) kwa zile zinazotoa taaluma ya ufundi zishiriki katika kutoa mafunzo kwa vikosi vya ujenzi,
(ii) Kueneza teknolojia rahisi na yenye gharama nafuu,
(iii) Kuandaa ramani za gharama nafu,
(iv) Kujenga nyumba za mfano kwa kushirikiana na wananchi, na
(v) Kuhamasisha jamii zinazozunguka vyuo zenye makazi duni kuboresha makazi yao.

**2.2.5 Mkoa**

Mkuu wa Mkoa atakuwa Balozi wa Kampeni ya Kuboresha Makazi ili kuhakikisha Kampeni inatekelezeka. Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa kupitia wataalam wa Maendeleo ya Jamii wataratibu utekelezaji wa kampeni ngazi ya Mkoa.

Majukumu ya Mkoa ni :-

(i) Kutambua na kushawishi wadau wataoweza kuchangia Kampeni,
(ii) Kuhakikisha utekelezaji wa Kampeni unafanyika kulingana na Sera na Miongozo,
(iii) Kusimamia utekelezaji wa kampeni katika ngazi ya Mkoa na mamlaka za Seriikali za Mitaa,
(iv) Kufuatilia utekelezaji wa kampeni, na
(v) Kujumuisha taarifa za utekelezaji wa kampeni kutoka Halmashauri na kuwasilisha OR-TAMISEMI.
(vi) Kuteua mabalozi wa Kampeni ngazi ya Wilaya

**2.2.6 Halmashauri**

Halmashauri zitakuwa na majukumu yafuatayo:-

(i) Kuhakikisha utekelezaji wa Kampeni unafanyika kulingana na Sera na Miongozo,
(ii) Kutambua na kushawishi wadau wataoweza kuchangia Kampeni,
(iii) Kusimamia utekelezaji wa kampeni katika ngazi ya Kata na Vijiji,
(iv) Kutenga bajeti ya utekelezaji wa Kampeni,

(v) Kutambua na kushawishi wadau wataoweza kuchangia Kampeni
(vi) Kutao ushauri wa kiufundi kwa jamii wakati wa utekelezaji wa Kampeni
(vii) Kufuatilia utekelezaji wa kampeni, na
(viii) Kujumuisha taarifa za utekelezaji wa kampeni kutoka Kata na kuwasilisha Sekretariati ya Mkoa.

Aidha, katika ngazi ya Wilaya/Halmashauri, Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya na Madiwani kwa nafasi zao watakuwa Mabalozi wa Kampeni kwenye maeneo yao ili kuhakikisha Kampeni inatekelezeka. Uteuzi wa Mabalozi wa Kampeni ngazi ya Kata utafanywa na Mkuu wa Wilaya husika.

### 2.2.8 Kata

Wataalam wa maendeleo ya jamii ngazi ya Kata watawajibika na:

(i) Kuweka mikakati ya utekelezaji wa Kampeni kwa kushirikiana na viongozi wa wilaya, kata, mitaa, vijiji na wadau wa maendeleo katika eneo husika.
(ii) Kuhamasisha jamii kurejesha mifumo ya asili ya kusaidiana katika shughuli za maendeleo kwa mtu mmoja mmoja hususani katika ujenzi wa nyumba bora
(iii) Kutafuta wadau watakaowezesha upatikanaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba bora.
(iv) Kuhimiza matumizi ya teknolojia rahisi na ujenzi wa gharama nafuu.
(v) Kuratibu Kampeni.
(vi) Kuandaa taarifa na kuwasilisha ngazi ya Halmashauri

### 2.2.8 Asasi za Kiraia

Asasi za Kiraia zinategemewa kushiriki kampeni hii kwa kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kushirikiana na wataalamu wa Maendeleo ya jamii Kutoa hamasa ya ujenzi wa nyumba bora,
(ii) Kuwezesha rasilimali fedha, vifaa vya ujenzi, teknolojia, elimu kwa jamii na hata kujenga nyumba za mfano.
(iii) Kushirikiana na wataalamu wa Maendeleo ya jamii (kuielimisha) jamii juu ya umuhimu wa nyumba bora za gharama nafuu na teknolojia rahisi

### 2.2.9 Sekta Binafsi

Sekta binafsi kwa kuzingatia umuhimu wake kwa kila ngazi itakuwa na majukumu yafuatayo: -

(i) Kuchangia maendeleo ya jamii (Corporate Social Responsibility) itachangia kwa kujenga nyumba za mfano kwa wahitaji,

(i) Kuchangia rasimali za ujenzi kama saruji, bati, nondo, milango na madirisha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zitakazojengwa na jamii kusaidia wenye mahitaji maalum waliotambuliwa

(ii) Kuwezesha upatikanaji wa saruji, bati, nondo na vifaa vya mabomba jirani na makazi ya watu kwa kufungua maduka ya vifaa vya ujenzi.

## SURA YA TATU

## UFUATILIAJI, TATHIMINI NA UTOAJI WA TAARIFA

### 3.1 Ufuatiliaji

Ufuatiliaji utawezesha kupata taarifa za utekelezaji na hatua zilizofikiwa katika ujenzi wa nyumba bora. Mtalaam atahakikisha kuwa utekelezaji umefikia malengo. Masuala ambayo mtaalam atatakiwa kufuatilia ni pamoja na matumizi ya raslimali zilizopangwa kutumika katika Kampeni, wadau watakaoshiriki na uwepo wa nguvu kazi katika kufanikisha utekelezaji wa Kampeni

### 3.1.1 Njia zitakazotumika katika ufuatiliaji

(i) Usimamizi wa Kampeni
(ii) Kufanya tathmini ya nyumba zilizojengwa.
(iii) Kuwahoji wahusika wa Kampeni
(iv) Majadiliano ya ana kwa ana
(v) Mikutano ya hadhara na wananchi
(vi) Kupitia taarifa mbalimbali za utekelezaji wa Kampeni kwa ngazi husika

### 3.2 Tathmini

Tathmini itafanyika katikati ya Kampeni mwaka mmoja na nusu (Juni 2021) na mwisho wa utekelezaji Juni 2023) ili kupima mafanikio ya utekelezaji wa Kampeni. Kila Halmashauri itaweka malengo (target) ya kufikia kwa kutumia takwimu za idadi ya makazi duni zilizopatikana katika hatua ya kwanza kupima mafanikio kwa kuangalia (viashiria) mfano idadi ya makazi duni kabla ya kampeni na idadi ya makazi yaliyoboreshwa baada ya kampeni.

### 3.2.1 Masuala yatakayotathiminiwa

Wataalam wakati wa kutathimini utekelezaji wa Kampeni wataangalia yafuatayo: -

(i) Umuhimu wa Kampeni kwa walengwa.
(ii) Ufanyikaji wa kampeni na iwapo imefanyika kwa wakati,
(iii) Jinsi kampeni ilivyofanyika kulingana na raslimali
(iv) Uendelevu wa kampeni
(v) Matokeo mazuri na hasi ambayo yametokea na hayakutarajiwa katika kampeni

### 3.3 Utoaji wa Taarifa za Utekelezaji wa Kampeni

Kwa Mujibuwa Kifungu 55(4) cha Sheria ya Bajeti Na.11 ya mwaka 2015 na

Kanuni 30(3) ya Sheria hiyo, inaelekezwa utoaji wa taarifa za utekelezaji wa bajeti. Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wanatakiwa kuandaa taarifa za utekelezaji wa Kampeni ya ujenzi wa nyumba bora kwa kila robo mwaka na kuwasilishwa katika Mamlaka husika. Wataalam wa Maendeleo ya Jamii wa Sekretariati za Mikoa wataunganisha taarifa husika na kuwasilisha OR-TAMISEMI

### 3.4 Uenezi wa Kampeni

Ili kueneza Kampeni katika ngazi ya kitaifa vyombo vya habari vitatumika ikiwemo Mitandao ya Kijamii, Luninga, Redio za kitaifa na kijamii na magazeti. Inashauriwa kwa zile Halmashauri zenye vyombo vyake vya habari ni vyema zikatumika ikiwemo redio za kijamii kwenye maeneo inapofanyika Kampeni.

## 4.0 HITIMISHO

Wataalam wa Maendeleo ya jamii, Wizara, Sekretariati za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Asasi za Kiraia zinaelekezwa kuzingatia Mwongozo huu wakati wa kufanya Kampeni ya kuboresha Makazi katika jamii. Vilevile zinaelekezwa kuongeza ushiriki katika kutekeleza Kampeni hii. Wataalam wa Maendeeo ya jamii wanaelekezwa kuratibu uandaaji na utekelezaji wa Kampeni.

## Viambatisho

### Kiambatisho Na. 1: Dodoso la Kukusanyia Takwimu za Awali za Kiuchumi na Kijami (Ngazi ya Kijiji/Mtaa)

1. Jina la kijiji/ Mtaa.............................
   Kata.............................Wilaya.................... Mkoa........................
2. Idadi ya Vitongoji...............................................
3. Majina ya vitongoji..............................................
4. Umbali kutoka makao makuu ya wilaya........................
5. Ainisha Makabila yaliyopo kwenye kijiji.....................................
6. Ukubwa wa eneo........... Eneo lilitengwa kwa ajili ya makazi..................
7. Idadi ya Wakazi............................. Me...............Ke........................ Wenye uwezo wa kufanya kazi................., Idadi ya Vljana.................., Idadi ya Watoto................., Idadi ya Wazee..............
8. Idadi ya Kaya Kivitongoji ...................................)
9. Idadi ya Nyumba Bora jumla na kivitongoji...........................................
10. Idadi ya Makazi duni jumla na kivitongoji....................................
11. Umiliki wa nyumba nyumba bora Kwa jinsi, Jumla na kivitongoji...............
12. Idadi ya Kaya zinazomilikiwa na watoto na hali yake...................... (orodhesha kwa majina)
13. Idadi ya kaya zinazomilikiwa na wazee na hali yake.....................................................
14. Idadi ya kaya zenye kipato cha chini zilizotambuliwa na TASAF.................... Ikiwezekana pata na orodha yake.
15. Idadi ya wakazi wenye hati milki za kimila kwa mchanganuo wa jinsi..................................
16. Huduma za Kijamii zilizopo kijijini........................(Maji, Umeme, barabara, vituo vya kutolea huduma za afya, shule ya Msingi, Shule za Sekondari nk)
17. Madhehebu ya dini yaliyopo kwenye jamii.........................................
18. Shughuli za Kiuchumi zilizopo kijijini.....................................................
19. Uwepo wa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi........... ..........
20. Taasisi zilizopo Kijijini.........................................................
21. Mashirika ya Yasiyo Kiserikali yanayofanya kazi kwenye jamii.......................
22. Taja mashirika yanayofanya shughuli za kuboresha makazi kama yapo...........................

## 5.2 Kiambatisho Na. 2: Zana za Kukusanyia Taarifa Zinazohusiana na Kuboresha Makazi

### (a) Ramani ya Rasilimali (Resource Map)

Ramani ya rasilimali ya jamii ni mbinu inayotumika kuonesha upatikanaji, mgawanyo, kufikika na matumizi ya rasilimali; hali ya ardhi, makazi na shughuli za kijamii zinazofanyika katika jamii kulingana na matazamo wa jamii yenyewe.

**Matumizi**

- Kutambua na kuchambua mahusiano yaliyopo kati ya rasilimali zilizopo kwenye jamii, makazi na shughuli za uzalishaji. Na zoezi la uboreshaji makazi litasaidia kutambua endapo rasilimali za ujenzi wa nyumba bora zinapatikana kwenye jamii na ni zipi zinapatikana nje ya jamii.
- Itawezesha jamii na mwezeshaji kupata aina ya rasilimali zilizopo.
- Itasadia kutambua changamoto za kuboresha makazi, uwezekano na fursa zilizopo katika kuboresha makazi.

**Faida**

- Itaonesha mtazamo wa jamii kuhusu mazingira yao na rasilimali zilizopo zinavyoweza kutumika katika kuboresha makazi yao

**Namna ya Kuandaa**

Washiriki waelekezwe kuchora alama maalum kwa kadri wanavyofahamu wao. Ramani ya rasilimali inaweza ikaandaliwa chini ya ardhi kwa kutumia matawi ya miti, vizibo, vijiti, kokoto, makopo kuonesha rasimali, taasisi, shughuli za kiuchumi, changamoto mbalimbali zilizopo kwa mtazamo wa jamii yenyewe. Kilichooneshwa kwenye ardhi kihamishie kwenye karatasi kubwa.

### (b) Kataa ya Njia (Transect Walk)

Kataa ya Njia ya matembezi yaliyopangwa kukatisha eneo ambalo kampeni ya kuboresha makazi itafanyika kwa ajili ya kuangalia hali ya makazi na kuthibitisha aina za rasilimali zilizopo katika jamii zinazoweza kutumika katika ujenzi wa nyumba Bora. Zoezi hili litahusisha utambuzi wa aina ya udongo kama unafaa kwa kutengeneza matofali, eneo yanapopatikana mawe ya kujengea, eneo unapopatikana mchanga wa kujengea, upatikanaji wa nishati za kuchomea

matofali, uwepo wa mpango wa matumizi bora wa ardhi na mpangilio wa kaya. Kama Kijiji/Mtaa hakina Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi, wahimizwe kufanya kujenga nyumba kwa mpangilio ulio mzuri kwa kuweka mitaa ili kuwepusha makazi holela. Wakati wa Matembezi mwezeshaji ataangalia, atauliza maswali na kikundi kitaandaa mchoro. Matembezi hufanyika kwa kushirikiana Wawezeshaji na Wana jamii.

**Faida**

- Itasaidia kutambua fursa na changamoto za kuboresha makazi
- Itasaidia kutambua teknolojia za ujenzi wa nyumba zinazotumika katika jamii.
- Itasaidia kuthibitisha yaliyosemwa kwenye ramani ya rasilimali kuhusu rasilimali zinazopatikana na changamoto zilizotajwa kwenye majadiliano ya kundi lengwa.

**Changamoto**

- Unaweza usipate walengwa wanaofaa kwenye majadiliano

**Matokeo ya Kataa ya Njia**

- Itasaidia kuelewa aina ya makazi katika jamii.
- Itasaidia kuibua teknolojia za ujenzi wa nyumba zilizopo kwenye kijiji.
- Itasaidia kuthibitisha hali ya makazi ya wenye uhitaji kama ilivyojitokeza kwenye majadiliano.
- Itasaidia kuona namna nyumba zitakavyopangwa.
- Itasadia kuona au kuthibitisha huduma za kijamii zilizopo

**Namna ya kufanya Kataa ya Njia**

- Tambua watu wanaoifahamu vizuri jamii na eneo lake na wawe tayari kutembea mwendo mrefu.
- Jadili na wahusika lengo la kufanya kataa ya njia na kukubaliana eneo litakalopitiwa
- Kukubaliana masuala muhimu yatakayoangaliwa kwenye kata ya njia mfano makazi, udongo, rasilimali za ujenzi nk
- Taarifa na mchoro huandaliwa wakati mnapoendelea na kataa ya njia.

**(c) Majadiliano ya Kundi Lengwa (Focus Group Discussion)**

Majadiliano ya Kundi lengwa ni majadiliano ya kina na mahojiano na kundi

dogo kwenye suala ambalo linahitaji maoni ya kundi husika. Kimsingi katika kukusanya taarifa au takwimu za kampeni hii inaweza kutumika kuelewa mwitikio wa jamii kusaidia kujenga nyumba za wahitaji, au namna vikundi vya akiba na mikopo vinavyoweza kutumia fursa walizo nazo kuboresha au kujenga nyumba bora. Majadiliano ya kundi lengwa yanaweza yakatumika kuibua mila na desturi zilizo nzuri zitakazofanikisha kampeni. Mara nyingi Majadiliano hayo yanahusisha kikundi cha kati ya washiriki 6 hadi 10.

Zana ya majadiliano ya Kundi lengwa inamwezesha mwezeshaji kuelewa kundi, mwitikio wao katika suala linalojadiliwa, maoni na mitazamo ya washiriki.


Mwezeshaji aulize maswali machache ya kuibua mjadala na ajitahidi kutoingilia wakati washiriki wanajadili. Aingilie pale tu ambapo mjadala umepotea na kutoka nje ya mada au kutoendelea.

Ukiwa na kinasa sauti unaweza kurekodi majadiliano au unaweza kuandika kidogo; lakini pata ridhaa ya washiriki; hasa ukitaka kutumia kifaa cha kurekodia.


**(d) Mchoro wa Mahusiano (Venn Diagram)**

Ili kuelewa mahusiano, ushawishi na nguvu kati ya mtu, kikundi na taasisi kwenye jamii ambazo zitasaidia kufanikisha kampeni utatumia michoro ya maboksi yenye ukubwa tofauti tofauti yatakayoonesha uwezo na nguvu ya ushawishi kwa mtu binafsi, kikundi au taasisi kama shule, kanisa au msikiti. Umbali au muungano wa maboksi kwenye mahusiano itaonesha jinsi taasisi hizo zinavyoweza kushirikiana au kutofautiana katika Kampeni. Ukitumia miduara (Venn Diagram) zitaonesha jinsi taasisi hizo zinavyoweza kuhusiana.


Mahusiano ya kitaasisi yatamuonesha mwezeshaji ni taasisi zipi azitumie au watu katika kufanikisha Kampeni.




front side elevation



right side elevation




rear side elevation





ground floor plan

TYPE A


PROPOSED NYUMBA YA GHARAMA NAFUU 2019




front side elevation



right side elevation




rear side elevation





ground floor plan

TYPE B


PROPOSED NYUMBA YA GHARAMA NAFUU




front side elevation



rear side elevation




right side elevation





ground floor plan

TYPE C


PROPOSED NYUMBA YA GHARAMA NAFUU




front side elevation



right side elevation



rear side elevation




ground floor plan

TYPE D

PROPOSED NYUMBA YA GHARAMA NAFUU